# KUKATA TAMAA

Je, umewahi kuwa na matumamini makubwa? Labda kwa kuwa na matarajio na shuku iliyotokana na kujua kwamba kuna jambo fulani zuri sana linakaribia kutokea, kisha mara moyo ukavunjika nukta ile ulipogundua kuwa matumaini yako yameyeyuka. Labda pengine ulitegemea kupata ajira mpya. Au ulitegemea kwamba mchumba wako atakuja kutoa posa na badala yake akavuta muda? Yawezekana ulikuwa unategemea ufadhili? Ulikuwa umetoka kuhesabu kuku na ukajikuta unaanza kuhesabu machozi. Sote tumekabiliwa na hali ya kukata tamaa za aina tofauti tofauti. Yawezekana kuna watu wamekusababisha ushindwe? Mwanao, mchumba wako, timu yako ya mpira au Mhenga wako ameshindwa na kukuangusha. Ni vigumu kukabiliana na kuzoea hali ya kukata tamaa. Lakini kama wana wa Mungu tunatakiwa kujifunza namna ya kukabiliana na matarajio yanayoshindwa kutokea kama tulivyotegemea.

Namkumbuka Eliya na vita yake dhidi ya manabii wa Baali katika 1Wafal. 18. Mara baada ya kushinda vita yake dhidi ya mafundisho potofu alidhani sasa angeongoza harakati za uamusho na kuyaleta kwenye zizi la Mungu makabila kumi ya Kaskazini. Walakin hakukuwa na uongofu mkubwa. Na kwa kweli, siku kadhaa baadaye ni kama hakuna aliyejali. Ni kama watu waliyarudia maisha yao ya kawaida bila kuwa na wazo lolote la kumrudia Mungu! Na hali ilivyokuwa mbaya, Yezebeli alimtwika Eliya gharama zote 1 Wafal. 19:1-2.

Eliya akaahidiwa, akakataliwa, akakataliwa tena na zaidi sana Eliya alikuwa ameshindwa kukabiliana na hali yake ya kukata tamaa. Alikuwa ndiyo ametoka kumtetea Mungu na kudhihirisha kuwa Yahweh yupo na ya kuwa ndiye Mungu wa milele. Na badala ya watu kukubali ukweli, hawakujali. Kwa hiyo akakimbia, akajikuta yuko jangwani akimsihi Mungu amruhusu afe. Hebu na tuone kama masononeko haya yanaelekeana na sisi kwa mifano ifuatayo; Sijapata ajira ninayotaka,nami naacha kuendelea kutafuta vilevile. Kama anitosa kwa sababu ya msichana yule, basi naacha kuthubutu. Nisipopata ufadhili basi sina namna yoyote ya kupata elimu, kwa hiyo nitaacha. Kama siwezi kuwa mkamilifu katika Kristo, vilevile inabidi niache kujaribu. Vipi, mifano hii imezoeleka eti?

Katika 1Wafal. 19 Mungu anampa Eliya masomo kadhaa ili kumsaidia kukabiliana na hali ya kukata tamaa na ambayo yaweza kuwa msaada kwetu leo:

1)Si kila wakati Mungu atatupatia kila tunachokitaka, 19:4 Eliya alitaka kuwaokoa Israeli, lakini alikatishwa tamaa na kumwomba Mungu kuwa ni bora afe. Yawezekana na wewe kuna promosheni uliitaka, uliiombea, na ukajikuta nafasi hiyo imeenda kwa mtu mwingine huku hujui ni nani aliye na kiwango cha ubunifu mpya na ukajisemea moyoni ya kuwa nadhani inabidi nikate tamaa. Kumbuka Eliya hakufa! Na wala sisi hatutakiwi kuwa kama Eliya na kukata tamaa wakati mambo hayaendi vizuri. Mara nyingi mambo yanapogoma, zaidi sana tutambue ya kuwa yapo mema ajabu yanatungoja kesho, Habakuki 1:5.

2) Siku zote Mungu ni mwaminifu, hata nyakati zile ambazo tunakuwa tumekata tamaa katika kila kila jambo na kila mtu, mstari wa 5-8, Eliya alijisikia kutelekezwa na kuachwa peke yake, mstari wa 10,14. Hisia zake za upweke zilimtesa. Nafsi nyingi zimetelekeza familia zao, ajira, elimu na Mungu kwa sababu walijiona kama wanapambana peke yao katika vita ya maisha. Katika Mstari wa 5-8, Twajifunza ya kuwa hatuko peke yetu. Kama Mungu alivyokuwa mwaminifu kwa Eliya na akampatia mahitaji ya mwili na faraja, jambo lile lile lawezekana kwetu leo. Mungu yupo hapa kwa ajili yako na ataendelea kukupa yale

unayoyahitaji, Mathayo 6:33-34; 28:20; 6:8; Waebrania 13:5 “Maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba”

3) Katika kupambana na kukata tamaa, tunatakiwa kujua kwamba wakati fulani mahitaji ya mwili huhitajika kabla ya kushughulikia mahitaji ya kiroho, 1 Wafal. 19:5-8. Ikitokea kukata tamaa kukaachwa bila kudhibitiwa, kunaweza kuleteleza madhara makuwa mwilini. Kwa upande wa Eliya, yeye azira kula na akaamua kufanya ambacho wengi waliokata tamaa hufanya na jambo hilo ni kulala kila wakati. Alikata tamaa! Alitaka kufa na alilala akisubiri mauti imchukue. Katika aya hii zingatia, kabla Mungu hajamsaidia Eliya kiroho, kwanza alimsaidia kimwili. Tunatakiwa kulikumbuka somo hili tunapokuwa tuna jaribu kuwasaidia watu ambao wamekumbwa na kukata tamaa. Wakati fulani rohoni hakuwezi kutengamaa hadi tuwasaidie  mahitaji yao ya kimwili.

4) Siku zote tukumbuke kuwa nguvu ya kubadili maisha ya watu iko katika neno la Mungu, 19:9-13. Yawezekana Israeli walishuhudia miujiza mikubwa pale kwenye mlima Karmeli. Yawezekana walikubali waziwazi kuwa Yahweh ni mkubwa zaidi ya Baali. Lakini watu hawa hawakuwa wamesikia neno la Mungu kwa muda mrefu, na wengi wao hawakujua cha kufanya ili kumpendeza na Mungu. Kwa hiyo, walipotoka Kalmeli walienda majumbani kwao. Na sasa ndiposa Mungu anamwonyesha Eliya jinsi alivyoitiisha asili na akaonyesha kimbunga, matetemeko ya nchi na moto. Na ni wazi Eliya alifurahia. Lakini alipoongea naye kwa kunong’ona ndicho kilimzindua Eliya! Cha kujifunza kiko wazi na dhahiri kwa wale waliokata tamaa. Neno la Mungu ndilo liletalo amani, furaha na uelewa wa kiroho. Mtu anaposikiliza na kutii Neno la Mungu hapa ndipo uongofu wa kweli huchukua nafasi.

5) Katika kupambana na kukata tamaa, lazima utambue kuwa unagusa maisha ya wengi kuliko unavyoweza kufikiri, 19:4-8. Eliya alijua ya kuwa alikuwa mshindwa. Hata pamoja na nguvu za Mungu alizokuwa nazo hakuweza kuwashawishi Waisraeli hata wakatubu. Na hicho ndicho alichokuwa anataka kukifanya kwamba awaongoze watu wa Mungu wamrudie Mungu.  Kwa hiyo aliamini ya kuwa yeye ni mshindwa. Lakini Mungu akamwambia aende kumtia mafuta Hazaeli kule Shamu na Yehu kule Isareli , pamoja Elisha kama mbadala wake. Kisah Mungu akamkumbusha Eliya kwamba kulikuwa na nafsi za watu waaminifu aliojisazia Mungu wapata 7,000. Ukweli ni kwamba Eliya alishindwa kuona aina ya ushawishi aliokuwa nao. Na ndivyo nasi tulivyo leo. Tunaweza kukata tamaa hadi kufikia hatua ya kusadiki kuwa hatuivishi lolote hapa ulimwenguni au kwenye familia zetu, au kwa Mungu. Bado, uhalisia ni kwamba matunda yaliyo mengi tunayozaa hayaonekani, na siyo kazi yetu kuhakisha tunayaona!